

More past papers are available on <http://www.kenyaplex.com>

Kenya Methodist University Sarufi ya Kiswahili(KISW 001) (LSWA 091) Past Paper

MUDA: SAA MBILI

Maagizo:

Jibu maswali yote

Andika wingi wa sentensi zifuatazo kwa kukanusha.

(al. 4)

Panga lilitumiwa kukata ulili wenyewe.

Kiti kingenunuliwa, walimu wangeketi vizuri afisini.

Uganisha sentensi ukitumia O-rejeshi

(al. 4)

Kipora yule hudona mtama. Kipora mwenyewe atafungiwa kizimbani.

Ndizi hii itaoza. Ndizi hii itatupwa jalalani.

Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi ya 'na'.

(al. 4)

Ainisha aina za maneno katika tungo zifuatazo.

(al. 5)

Mkulima alikuwa akilima shambani

Mgonjwa wa ukimwi amelazwa juu ya mkeka.

Nomino zifuatazo ziko ngeli gani?

(al. 5)

Chai \_\_\_\_

Kulima \_\_\_\_

Majibwa \_\_\_\_

Tuzo \_\_\_\_

Uyoga \_\_\_\_

Taja aina mbili za vishazi na uvitolee mifano miwili miwili kwa kila moja.

(al. 6)

Andika sentensi zifuatazo kwa ukubwa:

(al. 6)

Mbuzi wa kike aliharibu mche wangu.

Njia hiyo nyembamba iendayo mbinguni

Mbu, mchwa na nzige ni wadudu waharibifu

Tunga sentensi za aina zifuatazo:

(al. 6)

Sahili

Ambatano

Changamano

Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo:

Ahidi

Unda

Piga

Ita

Lima

Eleza maana tatu zinazojidhihirisha kwenye sentensi hii.

(al. 3)

Rhoda alimpigia Juma mpira.

Andika kinyume

(al. 2)

Baba alicheka alipomwona mama.

Andika katika hali ya mazoea.

(al. 2)

Mtoto alimmua nyuni kwa kumpiga kichwani.

Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi tofauti ya kikomo.(al. 2)

Andika katika kauli iliyo mabanoni.

(al. 2)

Panya ali \_\_\_\_\_ (ua) nap aka (kutendwa)

Samba aliwa \_\_\_\_\_ - (ogopa) mbuzi. (kutendesha)

Akifisha:

(al. 2)

Njoo upesi baba alimwambia mwanaye

Ainisha viambishi katika kitenzi hiki.

(al. 2)

alimshonea